

**SWALI:** Tukisoma katika maandiko tunaona sehemu kadha wa kadha likitajwa neno "Torati na manabii". Sasa hii torati na manabii maana yake ni nini? Kwamfano Mathayo 7:12 inasema

*"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii".*

**JIBU:** Bwana Yesu aliposema Torati na manabii, alimaanisha Agano la kale, ambalo ndio limeundwa na vitabu vyta Musa (Torati), ambavyo ni vitano (5), Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. Pamoja na vitabu vyote vyta manabii, kama vile, Yeremia, Isaya, Danieli, Ezekieli, Hababuki, Amosi, n.k. hapa ikijumuisha pia, vile vingine kama Waamuzi, Zaburi, Ayubu, Wafalme, Mithali, Ruthu n.k. Ambavyo sio moja kwa moja vyta manabii, lakini vimebeba nabii za Mungu ndani yake.

Kwahiyo torati na manabii kwa ufupi ni lile agano lote la kale. Hivyo Pale Bwana Yesu alipokuwa anawafundisha juu ya kanuni za kufuata, alirejea biblia yao, akiwaambia kuwa kiini cha biblia hiyo ni UPENDO. Wala hakuna siri nyingine nyuma yake, Torati yote, pamoja manabii wote, walichokuwa wanahubiri ni Upendo, (Ambao umegawanyika, wa

Mungu na wanadamu)

Hata sisi wa leo tulio katika agano jipya, tunaposoma biblia yote tujue Ujumbe mkuu tunaoupata katika agano letu ni ule ule UPENDO. Na ndio maana Mtume Paulo alisema.

*1 Wakorintho 13:1 "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao.*

*2 Tena nijapokuwa na unabii, na kujuu siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi.*

*3 Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu".*

Hivyo na sisi, tunapaswa tuutafute huu, kwa bidii zote, ili tuonekane kuwa wakamilifu mbele za Mungu.

Shalom

Nini maana ya "Torati na manabii"?

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema,

Kwa maombezi/Ratiba za ibada/ Ushauri/ Maswali.

Piga namba hizi: **+255693036618 au +255789001312**

pia kama utapenda uyapate mafundisho haya kwa njia ya Whatsapp au email basi tutumie ujumbe kwenye namba hizo hizo. **Jiunge na magroup yetu ya whatsapp kwa kubofya hapa > WHATSAPP-Group**

### **Mada Nyinginez:**

*Nini maana ya "Roho za manabii huwatii manabii?"*

*NITAUPATAJE UPENDO WA KI-MUNGU NDANI YANGU?*

*JE UPENDO WAKO UMEPOA?*

*Maswali na Majibu*

### **Rudi nyumbani**

Nini maana ya "Torati na manabii"?

Share on:

WhatsApp